**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**(FASIHI)**
**JULAI/AGOSTI, 2013**
**MUDA: SAA: 2½**

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA SEKONDARI WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI MWAKA WA 2013

**Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**(FASIHI)**
**MUDA: SAA: 2½**

**<u>MAAGIZO</u>:**

(a) Jibu maswali **manne** pekee.
(b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
(c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki yaani; **Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi** na **Fasihi Simulizi** .
(d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU A: SAID A. MOHAMED**

**SWALI LA LAZIMA: (ALAMA 20)**

1. Ujenzi wa jamii mpya ni mojawapo wa maudhui ambayo mwandishi wa Riwaya ya Utengano ameshughulikia kwa undani. Thibitisha ukweli wa kauli hii.

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY M. AREGE**

2. Kwa kuzingatia Tamthilia ya Mstahiki Meya, eleza huku ukitolea mifano, mbinu alizotumia Mstahiki Meya kuudumisha uongozi wake. (alama 20)

3. "Si nyinyi nd'o mjuao wanangu! … nilikiona afadhali".
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

   (b) Taja na utolee mifano ya mbinu zozote mbili za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (alama 4)

   (c) Fafanua maudhui yanayorejelewa na dondoo hili. (alama 12)

**SEHEMU YA C:**

4. **USHAIRI**

Uungana mbia ni mui, katu siuwati wema,
Wewe ndiwe wangu bui, na Lousiwa ni mama,
Neno kwamba suijui, ni kupotosha heshima,
Siati kutenda wema, kaandama uadui.

Wema nambiwa na ndia, hadi bandari salama,
Hayo niliyasikia, wao wahenga wa zama,
Penye wema tajitia, nipate taadhima,
Siati kutenda wema, japo munganinunia.

Ni iwe kupawa mali, ya kuhadaa mtima,
Niandame ufidhuli, nitengane nao wema,
Hilo sitokubali, hapo waja wangasema,
Siati kutenda wema, ujapokuwa ni ghali.

Sitomcha kabaila, nganiteuza nache wema,
Muunganitia na jela, kisa imefanza huruma,
Haragwe lenu talila, pamoja na yenu sima,
Siati kutenda wema, japo tagoni talala.

Haufi mungaufisha, au hamipo karima,
Mola atauhusha, weleleapo kuzama,
Mimi ni huo maisha, hadi siku ya kiama,
Siati kutenda wema, nganitia mshawasha.

Wema ingawa mchungu, tajaribu kutotema,
Tautenda nenda zangu, niache wanaosema,
Malipo yangu kwa Mungu, hayo, yenu si, lazima,
Siati kutenda wema, kigharimu roho yangu.

(a) Ukizingatia beti **nne** za mwanzo, taja mambo ambayo hata mshairi akifanyiwa hawezi kuacha kutenda mema. (alama 4)

(b) Eleza jinsi mtunzi wa shairi hili alivyotumiwa uhuru wake. (alama 4)

(c) Mshairi alipata wapi ari ya kuzingatia wema? (alama 1)

(d) Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 2)

(e) Fafanua muundo wa ubeti wa pili. (alama 2)

(f) Andika ubeti wa mwisho katika lugha ya nathari. (alama 4)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
- (i) Mtima
- (ii) Kutotema
- (iii) Kigharimu roho yangu

**SEHEMU D:**

**HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**MKE WANGU – M.S.A**

5. (a) Anwani 'mke wangu' inasawiri yaliyomo katika hadithi husika. Jadili. (alama 10)

(b) Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii hii. (alama 10)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

6. **DAMU NYEUSI – KEN WALIBORA**

Eleza jinsi ubaguzi na unyanyasaji unavyosawiria katika hadithi hii. (alama 20)

AU

7. "Leo ni siku ya siku, siku ya nyani kufa ambapo miti yote huteleza".

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza tamathali za usemi zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Fafanua maudhui yanayorejelewa katika dondoo hili. (alama 12)

**SEHEMU E:**

**FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Taja sifa zozote **nne** za maigizo. (alama 4)

(b) Taja aina zozote **nne** za maigizo. (alama 4)

(c) Ni nini tofauti ya maigizo na hadithi. (alama 6)

(d) Eleza dhima ya maigizo kama utanzu wa fasihi simulizi. (alama 6)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com